# MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI - ZANZIBAR (ZURA)

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, imeanzishwa chini ya sheria Nam.7/2013 ikiwa na jukumu la kusimamia huduma za Maji na Nishati hapa Zanzibar.

ZURA kwa uwezo na Mamlaka iliyonayo chini ya kifungu nambari 16 (C) ya sheria Nam. 7/2013 inapenda kuwatangazia wananchi wenye sifa kujaza nafasi za ajira kama zifuatazo katika Afisi zake za Unguja na Pemba.

1. **MKAGUZI UMEME DARAJA LA II. Nafasi 2 – Nafasi 1 Unguja - Nafasi 1 Pemba.**

**Sifa za Muombaji:**

- Awe Mzanzibari
- Awe na Shahada ya kwanza/Stashahada ya juu au Shahada ya Uzamili katika fani ya Umeme au inayolingana kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

2. **MKAGUZI NISHATI YA MAFUTA DARAJA LA II. Nafasi 2 – Nafasi 1 Unguja - Nafasi 1 Pemba.**

**Sifa za Muombaji:**

- Awe Mzanzibari
- Awe na Shahada ya kwanza katika fani za Nishati ya Mafuta, gesi au inayolingana na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada

**3. MKAGUZI MAJI DARAJA LA II. Nafasi 1 Pemba.**

**Sifa za Muombaji:**

- Awe Mzanzibari
- Awe na Shahada ya kwanza/Stashahada ya Juu/ Shahada ya Uzamili katika fani za ya Uhandisi, Jiolojia ya Maji, Mazingira, au inayolingana kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada

**4. MCHUMI/MASOKO DARAJA LA II. Nafasi 1 Unguja**

**Sifa za Muombaji.**

- Awe Mzanzibari
- Awe na Shahada ya kwanza/Stashahada ya Juu/Shahada ya Uzamili ya Uchumi (Economics), Masoko (Marketing), Mipango ya Uchumi (Economic Planning), Usimamizi wa Kodi, au fani inayolingana kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

**5. MCHAMBUZI WA KOMPYUTA DARAJA LA II. Nafasi 1 Unguja**

**Sifa za Muombaji:**

- Awe Mzanzibari
- Awe na Shahada ya kwanza/Stashahada ya Juu/Stashahada ya uzamili ya Sayansi ya Kompyuta, Uhandisi wa Kompyuta au fani inayolingana kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta hasa katika uchambuzi wa mfumo.
- Awe na ujuzi wa kutengeneza mifumo (system development) kwa kutumia Java, C na C ++.
- Awe na ujuzi katika mifumo ya kimtandao (networking) na hifadhi data (Database) ikiwemo Cloud Database.
- Awe na uwezo wa kutengeneza Graphics.
- Awe na ujuzi wa Mobile Applications kama Android Application

- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

6. **DEREVA DARAJA LA III. Nafasi 2 - Unguja**

**Sifa za Muombaji:**

- Awe Mzanzibari
- Awe na cheti cha kidato cha Nne (F.IV) aliyefaulu na kupata leseni ya udereva kutoka katika taasisi inayotoa leseni inayotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Uzoefu wa kazi ni sifa ya ziada.

## TAARIFA ZA JUMLA

Kwa waombaji wote watakaopata bahati ya kuchaguliwa kutafanyika usaili katika ofisi za ZURA zilizopo Maisara Zanzibar.

Muombaji yeyote atakaechaguliwa anatakiwa awe tayari kufanya kazi katika Afisi yoyote ya ZURA.

## TAREHE YA MWISHO WA MAOMBI

Maombi yataanza kupokelewa kuanzia leo tarehe 04/12/2018 na tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 17/12/2018.

## NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Waombaji wote wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi iliyoandikwa kwa mkono katika ofisi za ZURA na kuambatanisha na vivuli vya taarifa zifuatazo;

1. Vivuli vya Vyeti vya kumalizia masomo
2. Maelezo Binafsi (CV)
3. Cheti cha kuzaliwa
4. Picha mbili za paspoti zilizopigwa karibuni
5. Kitambulisho cha Mzanzibari

Maombi yote yawasilishwe katika anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)**

**S.L.P 2238, GHOROFA YA PILI, JENGO LA MFUKO WA BARABARA**

**MAISARA**

**ZANZIBAR**

**KWA WALE WALIOKO PEMBA MAOMBI YA YAPELEKWE AFISI ZA ZURA ZILIZOPO TIBIRINZI, CHAKECHAKE - PEMBA.**

**ANGALIZO:**

MAELEZO ZAIDI KUHUSIANA NA TANGAZO HILI FUATILIA KATIKA TOVUTI YA MAMLAKA **www.zura.go.tz,** NA GAZETI LA ZANZIBAR LEO LA TAREHE 05/12/2018.